# NAFASI ZA KAZI - UDEREVA

## MTIBWA SUGAR ESTATES LIMITED

## 16 JULAI 2025

1. **Utangulizi**

   Mtibwa Sugar Estates Limited ni kampuni inayojishughulisha na uzalishaji wa miwa na utengenezaji wa sukari katika eneo la Mtibwa – Turiani – Mvomero – Morogoro – Tanzania.

   Sifa mojawapo ya Mtibwa Sugar ni kufanya kazi kwa ushirikiano (teamwork). Mtu yeyote anayefanikiwa kuwa miongoni mwa wafanyakazi wa Mtibwa Sugar anakuwa mwanafamilia wa Mtibwa Sugar na hatajuta kwa maamuzi yake hayo kwani atapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wafanyakazi wenzake na Utawala kwa ujumla. Pia Mtibwa Sugar inajali kukuza vipaji na fani mbalimbali kwa wafanyakazi wote.

2. **Nafasi za kazi ya Udereva (nafasi 22)**

   Mtibwa Sugar inakaribisha maombi ya kazi kwa ajili ya nafasi za udereva wa magari ya kubeba wafanyakazi (labour trucks) na madereva wa magari makubwa ya kubinua mizigo (dumper trucks) ndani ya eneo la Mtibwa Sugar.

3. **Sifa za mwombaji**

   i. Awe Mtanzania
   ii. Awe na umri usiozidi miaka 40
   iii. Awe na leseni hai ya udereva inayoruhusu kuendesha malori au magari makubwa ya abiria.
   iv. Awe tayari kuishi Mtibwa
   v. Awe tayari kuanza kazi kati ya Mwezi Agosti na Septemba 2025
   vi. Awe na uzoefu wa kazi ya udereva kwa uchache miaka 5 (mitano)
   **vii.** Awe hana rekodi ya makosa ya jinai au kukutwa na hatia mahakamani katika makosa ya barabarani.

CamScanner

4. **Namna ya kutuma maombi na Viambatanishi**

Maombi yote yatumwe kwa barua pepe Hr@mtibwa-sugar.co.tz au yapelekwe katika ofisi za HR - MTIBWA au yatumwe kwa njia ya POSTA. Mwombaji aambatanishe wasifu (CV), picha yake ya hivi karibuni (passport size), leseni ya udereva, cheti cha mafunzo ya udereva, TIN, NIDA au kitambulisho kura na cheti cha kuzaliwa.

**Anuani**

**Meneja Rasilimali Watu na Utawala,**

**S.L.P 42, Mtibwa,**

**Morogoro.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25/07/2025.

Tunatanguliza shukrani

MTIBWA SUGAR ESTATES LTD
16 JUL 2025
P.O. Box 42, MTIBWA

Shani Christoms Mligo

Mkuu wa Idara

Rasilimali Watu na Utawala

CS CamScanner